# Mwongozo wa shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa

Shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa ni mipangilio ya shule za kitaalum ambayo inaweka pamoja **wanafunzi wenye uwezo wa juu na kipawa**.

Kujifunza pamoja na wenzao wa masomo wanao uwezo unaofanana husaidia maendeleo ya kitaalum na ustawi wa wanafunzi.

Wanafunza hufuata bado mtaala wa NSW, lakini walimu wanaweza kutumia mikakati maalum ya kufundisha kwa wanafunzi wenye uwezo wa juu na kipawa.

Katika kila darasa la fursa na shule ya upili iliyochaguliwa ya jinsia pamoja kutakuwa na idadi sawa ya nafasi zinazopatikana kwa wasichana na wavulana.

## Shule za upili zilizochaguliwa

Kuna aina 4 za shule za upili zilizochaguliwa:

- **shule za upili zilizochaguliwa kabisa** – hizi ni shule ambapo wanafunzi wote wamechaguliwa kutegemea mtihani wa uwekaji
- **shule za upili zilizochaguliwa kwa sehemu** – hizi ni shule zinazokuwa na mchanganyiko wa wanafunzi waliochaguliwa na wa eneo la karibu
- **shule za upili zilizochaguliwa za kilimo –** hizi ni shule zinazosisitiza masomo ya kilimo na wanafunzi wote wanachaguliwa kwa uwezo wao wa kitaaluma. Baadhi ya shule hizi pia hutoa bweni ambapo wanafunzi wanaishi shuleni
- **Aurora College** – hayo ni madarasa mtandaoni ya kuchaguliwa. Yanatolewa kwa shule za upili za serikali za eneo katika maeneo ya mashambani na vijijini.

## Madarasa ya fursa

Madarasa ya fursa ni ya wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa katika Miaka ya 5 na 6. Yanatolewa katika idadi ya shule za msingi za serikali kote NSW.

Aurora College hutoa madarasa ya fursa mtandaoni kwa wanafunzi wa mashambani na vijijini katika shule zao za msingi za eneo.

## Zinapatikana wapi?

Shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa yanapatikana katika jiji kuu, mkoa na vijijini za NSW. Angalia ramani hapo chini kupata shule karibu nawe.

- Pata darasa la fursa
- Pata shule ya upili iliyochaguliwa


CC BY

# Nitajuaje kama inafaa kwa mtoto wangu?

Je, mtoto wako:

- anapenda kujifunza
- ni mwenye dadisi sana
- anaonyesha kumbukumbu nzuri
- huuliza maswali magumu
- anahitaji marudio machache wakati wa kujifunza mambo mapya
- huonyesha njia za ubunifu za kufikiria
- anakuwa makini sana katika eneo lake la maslahi au shauku?

Ikiwa baadhi ya haya yanasikika kama mtoto wako, darasa la fursa au shule ya upili iliyochaguliwa inaweza kufaa.

# Niweke ombi jinsi gani?

Wazazi wanaweka ombi wakati wa kipindi cha maombi mtandaoni kwa: shsoc.education.nsw.gov.au

## Kuingia mwaka wa 2027 katika darasa la fursa au shule ya upili iliyochaguliwa

Kipindi cha maombi kwa kuingia mwaka wa 2027 ni kuanzia **6 Novemba 2025** hadi **20 Februari 2026.**

### Je, mtoto wangu yupo mwaka gani wakati ninapoomba nafasi?

**Madarasa ya fursa**

Wazazi hutuma ombi mtoto wao anapokaribia mwisho wa Mwaka wa 3 katika 2025 au mwanzoni mwa Mwaka wa 4 katika 2026.

**Shule za upili zilizochaguliwa**

Wazazi hutuma ombi mtoto wao anapokaribia mwisho wa Mwaka wa 5 katika 2025 au mwanzoni mwa Mwaka wa 6 katika 2026.

Jifunze zaidi kwenye tovuti yetu juu ya mchakato wa kutuma ombi na mahitaji ya ukaazi kwa nani anaweza kutuma ombi kwa madarasa ya fursa na nani anaweza kutuma ombi kwa shule ya upili iliyochaguliwa.

# Mtihani wa uwekaji

Baada ya kutuma ombi, mtoto wako lazima afanye mtihani. Kisha wanafunzi huchaguliwa kwa uwekaji kulingana na utendaji wao wa mtihani.

## Je, mtihani uko lini?

Mtihani unapatikana kwa muda wa siku 2:

**Mtihani wa shule za upili zilizochaguliwa: Ijumaa 1 Mei hadi Jumamosi 2 Mei 2026**

**Mtihani wa darasa la fursa: Ijumaa 8 Mei hadi Jumamosi 9 Mei 2026**

Wanafunzi huhudhuria siku moja tu ya mtihani na **hawahitaji** kuja na kompyuta yao wenyewe ili kufanya mitihani ya uwekaji kutumia kompyuta.

## Mitihani itafanyikwa wapi?

Mitihani hii itafanyika mara nyingi katika shule za upili za umma za NSW. Wanafunzi watapewa nafasi kwenye mahali pa kituo cha mtihani kutegemea wanapohudhuria shuleni. Wazazi wanahitaji kumchukua mtoto wao kwa kituo cha mtihani kwa siku ya mtihani.

## Ni nini katika mtihani?

Mtihani hutathmini jinsi gani wanafunzi wanavyoelewa vizuri kile wanachosoma, kusababu kwa kutumia hisabati na ujuzi wao wa kufikiri. Waombaji wa shule za upili zilizochaguliwa pia wanapata mtihani juu ya ujuzi wao wa kuandika.

Jifunze zaidi kwa: Mtihani wa uwekaji.

# Je, nitajua kuhusu matokeo ya mtoto wangu wakati gani?

Baada ya mtoto wako kufanya mtihani, utapokea barua pepe katika Muhula wa 3 ikiwa na utendajii wake wa mtihani na hatua zinazofuata. Mtoto wako akipewa nafasi, utapata maelezo kuhusu jinsi ya kujiandikisha.

# Mfano wa Upangaji Usawa

Mfano wa Upangaji Usawa husaidia wanafunzi wote kuwa na upatikanaji wa haki kwa shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa.

Chini ya Mfano, hadi nafasi 20% za wanafunzi katika kila darasa la shule ya upili iliyochaguliwa na la fursa zinafanyika kwa wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa:

- kutoka asili ya chini ya faida ya kijamii na kielimu
- wa Asili (Aboriginal) na/au wa visiwa wa Torres Strait
- kutoka maeneo ya mashambani na vijijini
- wenye ulemavu.

Nafasi zinazofanyika hutolewa kwa wanafunzi kulingana na ufaulu wao katika mtihani wa uwekaji.

Jifunze zaidi kwenye Upatikanaji wa Haki.

**Kusaidia wanafunzi wenye kipawa katika shule zote za serikali za NSW**

Shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa ni mojawapo tu ya njia ambazo Idara ya Elimu ya NSW husaidia wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa.

Wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa wanasaidiwa katika shule zote za serikali za NSW kufikia uwezo wao kamili. Jifunze zaidi kuhusu idara. Jifunze zaidi juu ya Sera ya Eilmu ya Uwezo wa Juu na wa Kipawa ya idara.

# Ukihitaji maelezo zaidi?

Angalia kurasa za tovuti zifuatazo kwa maelezo zaidi.

## Kurasa za tovuti kwa wazazi na walezi

- **Shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa:** education.nsw.gov.au/shs-oc
- **Shule za upili zilizochaguliwa:** education.nsw.gov.au/shs-yr7
- **Madarasa ya fursa:** education.nsw.gov.au/oc

## Kurasa za tovuti kwa wanafunzi

- **Maelezo ya shule za upili zilizochaguliwa na madarasa ya fursa kwa wanafunzi:** edu.nsw.link/shs-oc-students
- **Kutuma ombi kwa darasa la fursa:** Kitovu cha nyenzo za wanafunzi: edu.nsw.link/OChub
- **Kutuma ombi kwa shule ya upili iliyochaguliwa:** Kitovu cha nyenzo za wanafunzi: edu.nsw.link/SHShub

## Mitandao ya kijamii

Jiunge na vikundi rasmi vya Facebook vya idara yetu:

- **Uwekaji wa shule ya upili iliyochaguliwa:** edu.nsw.link/shs-fb
- **Madarasa ya fursa:** edu.nsw.link/oc-fb

## Wasiliana nasi

Wasiliana na Timu ya Kitengo cha Elimu Iliyochaguliwa (Selective Education Team) kwa:

**Email:** set@det.nsw.edu.au

**Simu:** 1300 880 367

**Huduma ya mkalimani wa simu: 131 450**

Ikiwa unahitaji mkalimani wa kukusaidia na swali lako tafadhali piga simu huduma ya mkalimani wa simu na umwambie mwendeshaji simu:

- lugha unayohitaji
- namba ya simu unayotaka kupiga simu.

Mwendeshaji wa simu atapiga simu kwa namba ya simu ya Timu ya Kitengo cha Elimu Iliyochaguliwa (1300 880 367) na atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.